Kutafiti Kuhusu Nguvu za Pamoja za Wanawake

ZALISHA. UZA. FANIKIWA.
UONGOZI WA WANAWAKE KIUCHUMI KATIKA MASOKO YA KILIMO

Matokeo na Mapendekezo

Februari 2013

Yaliyomo

- Vidokezo muhimu vya matokeo ya nguvu za pamoja za wanawake
- Mapendekezo ya utafiti
- Mikakati mipya ya watendaji wa maendeleo
- Mafunzo ya mikoani na kitaifa kwenye nchi za Ethiopia, Mali na Tanzania

Karibu

Mradi wa Utafiti kuhusu nguvu za pamoja za wanawake (WCA) ulianzishwa Desemba 2009 na na shirika la Oxfam, kwa ufadhili kutoka shirika la "Bill and Melinda Gates Foundation". Utafiti ulifanywa katika awamu tatu, na ulikusanya ushahidi wa jinsi mradi wa utafiti kuhusu nguvu za pamoja za wanawake unavyoweza kuboresha mapato ya wanawake wazalishaji wadogo wadogo, kuimarisha rasilimali zao na kuongeza uwezo wao wa kumiliki na kufanya maamuzi. Mradi pia uliwashirikisha wadau katika mazungumzo ya kuboresha mikakati na sera ili kuwezesha kwa ufanisi nguvu za pamoja za wanawake katika masoko ya kilimo. Katika haya maelezo, tunadokeza matokeo muhimu na mapendekezo kutoka awamu ya III ya utafiti, na kushirikisha taarifa za shughuli muhimu za wadau katika nchi tatu za mradi. Utafiti wa kitakwimu na wa kimaelezo ulifanywa katika sekta ndogo moja kwa kila nchi: Asali - Ethiopia, mboga za majani -Tanzania, na siagi ya "shea" - Mali. Ugunduzi huo umeweka wazi majibu ya maswali muhimu: Jinsi gani wanawake wazalishaji wadogo wadogo wanavyonufaika kutokana na nguvu za pamoja za wanawake? Jinsi gani vikundi vinavyowezesha wanawake kuvishinda vikwazo vya masoko? Ni wanawake gani wanaoshiriki katika shughuli za nguvu za pamoja na ni nani ambao hawashiriki? Ni mikakati gani ambayo ni muhimu sana itakayohakikisha wanawake wakulima wanapata faida? Matokeo haya yatawasaidia watendaji wa maendeleo kuboresha mikakati ya kuwasaidia wakulima wadogo wadogo na kuwashawishi wengine.

Picha: **Wazalishaji wa asali kutoka ushirika wa Meserethiwot katika mkoa wa Amhara,Ethiopia.** Kwa hisani ya : Berhanu Denu

Vidokezo muhimu vya matokeo ya nguvu za pamoja za wanawake (WCA)

Mafanikio ya kiuchumi na vizuizi

Wanachama wa WCA hupata mapato zaidi kuliko wanawake wanaofanya biashara peke yao.

Utafiti umeonesha faida muhimu za kiuchumi kwa wanawake wanaojiunga na vikundi vya nguvu za pamoja. Wanachama wanazalisha zaidi na bidhaa zao zina ubora zaidi, kwa hiyo wanapata mapato zaidi kutokana na wanachokiuza. Tanzania, wanachama wanawake wanapata karibu asilimia 70 zaidi ukilinganisha na wanawake wasio katika vikundi; Mali na Ethiopia wanachama wanapata asilimia 80 zaidi.

Vizuizi vya msingi bado vinawawekea mipaka wanachama wa WCA kushiriki katika masoko.

Nguvu za pamoja zinawaendeleza wanawake wazalishaji wadogo wadogo kupata mkopo na habari za masoko, wakati mafunzo na teknolojia ya kisasa yanaongeza ubora na uzalishaji zaidi. Lakini, umaskini wa muda, uwezo mdogo wa kutoka nje ya kijiji chao na desturi za kijamii bado zinawazuia wanawake wasiweze kufikia masoko ya mazao ya kilimo. Vikundi kwa nadra hushughulikia masuala haya, na husaidia wanawake zaidi katika uzalishaji na upatikanaji wa fedha kuliko katika mahusiano ya kimasoko.

Kujengeka kiuwezo

Wanachama wa WCA wameongeza umiliki wa kimaamuzi katika maeneo fulani fulani.

Katika nchi zote tatu, wanawake walio katika vikundi wana uwezo mkubwa zaidi wa maamuzi kuhusu mkopo, na matokeo haya yana umuhimu wanapokuwa pia ni wanachama wa vikundi visivyo rasmi. Vinginevyo, mabadiliko katika kujengeka kiuwezo yanatofautiana kadiri desturi za kijinsia zinavyotofautiana. Wakati, nchini Tanzania na Mali, wanawake wanachama wanafaidika kutokana na uhuru ulioongezeka wa kutoka sehemu moja hadi nyingine; Ethiopia wanafaidika kutokana na umiliki ulioongezeka kuhusu matumizi ya nyumbani. Nchini Mali wanachama wa WCA wamepata madaraka makubwa ya kuamua kuhusu matumizi ya mapato yanayotokana na kilimo, na sasa wanaombwa ushauri kuhusu maamuzi ya masuala ya kijamii na ya kishirika.

Mapato yatokanayo na masoko hayaleti hali ya kujengeka kiuwezo katika maeneo mapana

Wanachama wa WCA wanapata kipato zaidi kuliko wasio wanachama. Lakini, ni sehemu moja hadi tatu tu kati ya sehemu nane zinazotumika kupima mabadiliko katika umiliki wa maamuzi (tazama mbinu katika uk.2) ambapo wanawake wanachama wamejengeka kiuwezo kuliko wasio wanachama. Uanachama wa kikundi una matokeo kidogo kuhusu haki juu ya mali isiyohamishika. Kuwa mwanachama hakuimarishi kwa mpangilio uwezo wa wanawake kufanya maamuzi juu ya umiliki wa mali zisizohamishika. Lakini, baadhi ya wanawake huweza kufikia mali zisizohamishika za kibinafsi au za kijamii: KatikaTanzania, wanaume waliandikisha ardhi kwa ajili ya kilimo cha mboga za majani kwa majina ya wanawake na kule Mali wanawake walipata ardhi ili kupanda miti ya "shea"

Vikundi bora vya mfano

Vikundi rasmi na visiyo rasmi vyote vinafaa.
Mahusiano kati ya vikundi rasmi na visivyo rasmi ni ya muhimu katika ushiriki wa wanawake katika WCA. Vikundi visivyo rasmi vinawasaidia wanawake kujenga stadi za uongozi na kuweka akiba, wakati vikundi rasmi huweza kuzifikia pembejeo na huduma, na kushiriki kwa ufanisi zaidi katika masoko. Vikundi visivyo rasmi wakati mwingine hukua na kuwa vikundi rasmi vyenye ufanisi, na uanachama wa papo hapo wa vikundi visivyo rasmi unaweza kuongeza faida ya nguvu za pamoja zilizo rasmi. Hakuna kikundi cha aina moja kinachowanufaisha wanawake zaidi; Wanawake hujengeka kiuwezo katika maeneo mbalimbali, kutoka vikundi vya aina mbalimbali, na matokeo ya kujengeka kiuwezo mara nyingi ni makubwa zaidi kutokana na uanachama wa kikundi zaidi ya kimoja.

Vikundi vya wanawake pekee vinawezesha ushiriki mzuri kakika vikundi vya mchanganyiko.
Wakati faida za kiuchumi zinakuwa juu mara nyingi katika vikundi vya mchanganyiko kutokana na rasilimali kubwa zaidi, mitandao na ufikiaji mzuri wa usafiri bora, vikundi vya wanawake peke yao hutoa nafasi kwa wanawake kujenga stadi na moyo wa kujiamini, na hivyo kushiriki kwa ufanisi katika vikundi vya mchanganyiko. Vikundi vya wanawake peke yao au vikundi vinavyoongozwa na wanawake vinaweza kuondokana na hali ya faida zote kumilikiwa na wanaume (hali ya kawaida katika vikundi vya mchanganyiko ambapo wanaume huwa na nguvu ya uongozi). Uongozi wa kikundi ulio wazi na unaozingatia usawa wa kijinsia ni muhimu kwa ugawaji wa haki wa faida zinazotokana na juhudi za pamoja katika aina zote mbili za vikundi.

Uanachama wa Vikundi

Wanawake wenye uwezo zaidi ndio wenye mwelekeo wa kujiunga na vikundi
Wanachama wa WCA ni wenye umri mkubwa,walioolewa na wenye kutoka katika familia zenye uwezo, kwani wana majukumu machache ya kifamilia, wana muda zaidi, na uwezo wa kuwa na mali zisizo- hamishika na rasilimali. Tofauti ni kule Ethiopia, ambapo wanawake wasioolewa ndio wenye mwelekeo wa kujiunga na vikundi.

Kwa taarifa kuhusu Matokeo ya Awamu ya III, rejea Taarifa ya Utafiti wa Kimataifa wa Shirika la Oxfam (Oxfam International Research Report katika tovuti:

http://womenscollectiveaction.com/Phase+III

Mbinu za Utafiti

Mbinu za uchambuzi za kimaelezo na za kitakwimu zilitumika wakati wa awamu Awamu ya III ya Utafiti. Utafiti wa kimaelezo ulitumia mbinu ya visa mafunzo halisi kutambua, 'tofauti chanya' na kuchambua kwa kina visa 14 vya WCA katika nchi zote tatu.

Uchambuzi wa kitakwimu uliegemea kwenye mapitio ya tafiti za wanachama wa WCA wasiopungua 300 na za wasio wanachama wasiopungua 600 kwa kila nchi kwa kulinganisha manufaa ya kiuchumi na ya kujengeka kiuwezo kati ya hao wanaoshiriki katika vikundi na wanawake binafsi wanaofanya biashara katika sekta hizo hizo. Utafiti huo ulitazama madaraka ya wanawake katika maamuzi kwenye maeneo nane.[1]

Kwa taarifa zaidi kuhusu mbinu za huo utafiti wa Awamu ya III tembelea:

http://womenscollectiveaction.com/Phase+III

Kushoto- Kulia): **Mweka Hazina, Katibu na Mwenyekiti wa Kikundi cha Mboga cha Matumaini cha Wilaya ya Lushoto, Tanzania.** Kwa hisani ya: Martin Walsh

Manufaa ya Uanachama kwa Wanawake Wakulima Wadogo Wadogo Wanaojiunga na Vikundi vya Nguvu za Pamoja

Wanawake wakulima wadogo wadogo waliopo katika vikundi vya nguvu za pamoja wana…

- ✔ Mazao yenye ubora zaidi au wanazalisha zaidi.
- ✔ Wanapata kipato zaidi kutokana na mauzo ya mazao yao.
- ✔ Wana uhuru zaidi wa maamuzi kutumia mikopo yao.
- ✔ Wana muonekano wazi kama wanauchumi na wanaongeza ushawishi katika jumuia.
- ✔ Wana uwezo[japo kwa kiwango kidogo] zaidi wa kufikia masoko.

Lakini kujiunga na vikundi haina ulazima kwamba itasaidia wanawake…

- ✘ Kujengeka kiuwezo
- ✘ Kuwa na haki imara juu ya rasilimali zisizoweza kuhamishwa
- ✘ Kupata bei kubwa kwa bidhaa zao
- ✘ Kupata uwezo mkubwa ki-masoko (kwa sababu ya msisitizo kwenye uzalishaji)
- ✘ Kupunguza umaskini wa muda na vizuizi vya kufikia shughuli za ki-masoko

[1] Mbinu iliyotumika ilitokana na uzoefu wa "Kipimo cha Kujengeka Kiuwezo kwa Wanawake katika Kilimo"(Women's Empowerment in Agriculture Index "WEAI") kilichotayarishwa na Chuo cha Kimataifa cha Utafiti wa Sera za Chakula "IFPRI" na Mradi wa Oxford wa Umaskini na Maendeleo ya Watu (OPHI). Tazama: http://www.ophi.org.uk/policy/national-policy/the-women%E2%80%99s-empowerment-in-agriculture-index/kwa taarifa zaidi.

Mapendekezo yanayatokana na utafiti

Mapendekezo kwa Watendaji:

Lenga kwenye bidhaa ya thamani ya juu, sekta na teknolojia zilizo rafiki kwa wanawake. Kuwezesha shughuli za wanawake katika sekta ndogo za thamani kubwa, ambazo hazihitaji rasilimali ardhi (k.m. mazao ya miti, maziwa, nk), ni mlango wenye matumaini kwa mafanikio ya nguvu za pamoja za wanawake wakulima. Kutoa upenyo kwa teknolojia mpya, iliyo rafiki kwa wanawake, ikiunganishwa na mafunzo stahiki kunawezesha uingiaji wa wanawake kwenye vikundi na kuongeza thamani kwa njia ya uboreshaji wa thamani ya bidhaa. Misaada kwa ajili ya uimarishaji wa uzalishaji na uongezaji wa thamani lazima uendane na misaada kwa ajili ya vikundi kupata upenyo kwenye soko la bidhaa hizo.

Kuchambua mifumo ya masoko, kilimo na kaya. Watendaji lazima kuchambua majukumu ya kijinsia katika uuzaji / ununuzi wa bidhaa, mikondo ya soko na utendaji wake, ukiambatana na mahali vikundi vya nguvu za pamoja vilipo katika mnyororo wa thamani. Mifumo ya kilimo na jinsia na mwingiliano wa mahusiano ya kikaya pia yanahitaji kuchambuliwa, kwa kuwa haya yana uhusiano na mikakati na aina ya vikundi vitakavyofaa zaidi. Ingefaa, msaada kwa WCA uwe sehemu ya mkakati mpana kwa ajili ya kuleta mabadiliko katika mahusiano ya kijinsia katika sekta ndogo.

Wezesha shughuli za wanawake katika masoko mbali mbali. Kupunguza hatari na kuruhusu mabadiliko ya mipango, ni muhimu vikundi viwe na mahusiano na masoko mbalimbali badala ya kutegemea mnunuzi mmoja. Masoko ya ndani mara nyingi ni muhimu kwa wanawake wakulima wenye kipato kidogo kama masoko ya kitaifa na ya kimataifa. Vyama vya wazalishaji au mitandao ya vikundi huwa na wajibu mkubwa katika kukusanya bidhaa na kujadiliana bei na wanunuzi. Watendaji pia wanapaswa kutafuta fursa za kuwezesha wanawake viongozi wa vikundi na wanachama kushiriki kikamilifu katika kutengeneza mikakati ya masoko na katika kujadiliana bei na wanunuzi.

Tumia uzoefu wa vikundi vya nguvu za pamoja vilivyopo visivyo rasmi. Vikundi vya kiasili, pamoja na vikundi vya hivi karibuni vya kukopa na kulipa, vimetapakaa katika jamii yenye kipato cha chini vijijini; vikundi visivyo rasmi vya wafanyakazi pia vinapatikana. Vikundi kama hivi vinaweza kuunganishwa kwa ufanisi kwa vikundi vya mchanganyiko vya kimasoko. Watendaji wa maendeleo wanaweza kufanya kazi na vikundi vidogo vidogo visivyo rasmi kubuni shughuli za kiuchumi au kuwezesha uletaji wa bidhaa sokoni, kwa mfano kutoa usafiri.

Kuwa wazi katika uongezaji - thamani wa kikundi cha WCA au shughuli. Vikundi vya nguvu kazi vya pamoja ni njia madhubuti ya kupeleka pembejeo, mafunzo na teknolojia mpya, lakini shughuli ambazo hazionekani sana kama vile kukusanya nguvu kazi, kushirikishana ujuzi na taarifa, kupunguza uharibifu na gharama na kupunguza hatari, pia ni muhimu. Wakati wa kubuni mipango, watendaji ni lazima waangalie ongezeko la thamani halisi ya kila shughuli mpya, ni manufaa gani yatapatikana kwa wanachama wa vikundi, na jinsi gharama za muda na fedha zinavyolingana na hayo manufaa.

Zingatia matokeo ya kijinsia ya tabia za kikundi. Katika sekta ambazo zina wanawake wengi zaidi, au mahali ambapo wanawake wana uzoefu mdogo wa ki-chama, hususan wa vikundi mchanganyiko, vikundi vya wanawake peke yao vinaweza kufaa zaidi. Umri, hali ya kuoa au kuolewa, shughuli za kujipatia mahitaji muhimu ya maisha, majukumu ya nyumbani, muda walio nao na uwezo wa washiriki kutoka nje ya kaya zao ni mambo muhimu ya kuzingatia. Vikundi vidogo, ambayo havipo mbali mbali vinarahisisha ushiriki mzuri wa wanawake. Vigezo vyepesi kubadilika vinasaidia kuondokana na vizuizi vya moja kwa moja au visivyo wazi (k.m. kwa vigezo vya kujua kusoma na kuandika au kuwa na ardhi, au ada za juu sana) au aina fulani ya wanawake kwa mfano vijana ambao hawajaolewa.

Hakikisha wanaume wanakubali. Utayari wa wanaume kukubali na kusaidia katika ushiriki na uongozi wa wanawake kwenye vikundi vya masoko ni muhimu, kwa mfano kwa kufanya kazi za nyumbani au kutoa upenyo wa ufikiaji wa rasilimali kwa ngazi za kaya na za kijamii. Uhamasishaji wa wanaume ni muhimu kuwathibitishia manufaa ya WCA, na kujenga mazingira ya ushiriki bora wa wanawake katika vikundi.

Wezesha uongozi wa vikundi unaozingatia usawa wa kijinsia na uwajibikaji. Watendaji wa nje wanatakiwa kutia mkazo katika kujenga stadi ya ki-uongozi ya wanawake na kuimarisha uwezo wao wa uongozi katika vikundi mchanganyiko pia katika vikundi vya wanawake peke yao. Uongozi imara sharti uambatane na taratibu za uwajibikaji: Watendaji wa maendeleo wanatakiwa kufuatilia kwa ukaribu mwenendo wa kijamii ndani ya vikundi kupunguza hatari ya manufaa / faida kuchukuliwa na wanaume au wanawake wa ngazi za juu.

Hakikisha uendelevu wa WCA. Watendaji wa nje wanahitaji kufanya kazi na vikundi vya wanawake ili kupata upenyo ulio huru wa muda mrefu, wa wanawake kufikia rasilimali za kiasili na za kifedha zinazohitajika kuendeleza shughuli zao katika katika masoko mbalimbali, kuhakikisha kuwa mafanikio hayarudi nyuma au hayageuzwi.

Picha: Kushoto: **Bosena Atnafu, mwanachama wa kikundi cha *Serto Madeg* Ushirika wa Asali wa *Meserethiwot* katika Mkoa wa Amhara, Ethiopia.** Kwa hisani ya: Tarekegn Garomsa. *Kulia:* **Ramatou Couloubaly, Katibu Mtendaji wa Ushirika wa *Jigisèmè* wa Siagi ya Shea wa Koutiala cercle, Mali.** Kwa hisani ya: Edmond Dembele

Mapendekekezo kwa watunga sera

Boresha sera za kitaifa zinazotegemeza WCA. Kanuni wazi za kisheria za usawa wa ushiriki na manufaa yanayotokana na ushirika na aina nyingine za vikundi zinahitajika ili kutegemeza WCA yenye ufanisi. Mahali ambapo kanuni hizi tayari zipo, zinahitajika zifahamike kwa umma Katika ngazi za taifa na za jamii miongoni mwa watendaji wa maendeleo. Katika sehemu ambazo mapengo ya kijinsia yanaendelea kuwepo katika ushiriki kwenye mashirika rasmi ya kimasoko, mashirika ya kiserikali yanahitaji kukubaliana malengo ya kupunguza mapengo haya. Nafasi pia sharti zilindwe kwa mashirika yasiyo rasmi ambapo wanawake wengi wapo, na taratibu za kuimarisha mahusiano kati ya mashirika yaliyo rasmi na yasiyo rasmi. Watunga sera pia wanahitaji kuzingatia utegemezaji kwa vikundi vyenye mifumo inayonyumbulika kwa urahisi, upunguzaji wa gharama za uandikishaji na urahisishaji wa taratibu za vikundi.

Hakikisha uratibishaji wa ndani wa shughuli na ushirikishaji wa ujuzi. Kuelimishana kuhusu mashirika yaliyopo na msaada wanaopata kutoka kwa watendaji tofauti tofauti ni muhimu ili kujenga mahusiano na kuepuka kufanya shughuli zinazofanana katika eneo moja. Uongozi wa wilaya, mashirika ya ushirika katika jamii na ofisi za usawa wa kijinsia zinaweza kufanya kazi nzuri katika kuhamasisha mbinu stahiki za kuimarisha WCA.

Kupitia sera pana zinazoathiri ushiriki wa wanawake katika nguvu za pamoja na katika ujenzi wa uwezo wa wanawake vijijini. Uingiliaji kati wa kisera unahitaji pia kufanyia kazi mtazamo na imani zilizojikita kwa undani pamoja na mapengo ya kijinsia ya rasilimali, kwa mfano kwa kupitia uimarishaji wa haki za ardhi kwa wanawake na uandikishaji wa ardhi wa pamoja au wa mtu mmoja mmoja na mapitio ya sheria ya familia na haki ya umiliki wa rasilimali.

Kuanzisha mikakati mipya ya kuwanufaisha wakulima wanawake

Watendaji wa maendeleo hutumia idadi ya mikakati imara kuwashirikisha wanawake kwenye nguvu za pamoja na kuongeza mafanikio wanayoweza kuyapata katika vikundi vya WCA. Chini, tumechagua mifano ya shughuli zenye mwelekeo wa mafanikio kutoka nchini Ethiopia, Mali naTanzania vilivyopelekea kupata matokeo mazuri kwa wanawake kupitia nguvu za pamoja kwenye masoko.

Kubadilisha sheria ndogo ndogo ili kuongeza uanachama

Sheria za ushirika katika baadhi ya wilaya za mkoa wa Amhara nchini Ethiopia sasa zinaruhusu uanachama wa mume na mke kuliko wa mwanachama mmoja kwa kila kaya. Haya mabadiliko, yakiunganishwa na shughuli nyingine, yameongeza kwa kiwango kikubwa uanachama wa wanawake kwenye mashirika rasmi na kubadilisha mtazamo wa majukumu ya wanawake katika sekta ya asali.

Kupata rasilimali za kijamii

Kwa kuwashawishi viongozi wa kijamii, vikundi vya wanawake wanaouza siagi ya “shea” nchini Mali wameweza kupata upenyo wa kupata mali zisizohamishika na rasilimali kuendeleza shughuli zao katika sekta ndogo. Wanawake wamepewa kati ya hekta mbili hadi tatu za ploti za ardhi na viongozi wa jamii kwa ajili ya kilimo cha “shea” na wanaume pia wanapanda miti katika mashamba yao.

Kujenga mahusiano na masoko ya ndani ya thamani kubwa

Ushirikishwaji kwa shirika mwavuli la Ushirika wa Wafanya Biashara la Usambara Lishe (Usambara Lishe Trust) la Tanzania kumewezesha vikundi vya WCA kufikia masoko ya mbali, ya thamani kubwa kwa kulima mboga za majani za aina mbali mbali, kuendana na mabadiliko katika uhitaji. Kuwekeana mikataba na masoko makubwa yaliyoko mijini, na kuhakikisha wanawake wanachama wanapata malipo moja kwa moja na wanapata mafunzo ya masoko, hivi vyote vimekuwa ni vipengele chanya vilivyoongezea ufanisi.

Maelezo zaidi kuhusu hii na mikakati mingine yanaweza kupatikana katika visa mafunzo vya nchi husika, vinapatikana katika: **http://womenscollectiveaction.com/Case+Studies**

Semina za Kikanda na Kitaifa nchini Ethiopia, Mali na Tanzania

Mwezi Septemba na Oktoba 2012, Oxfam na washirika wake waliandaa semina za kitaifa katika kila nchi ya nchi tatu zilizolengwa. Watafiti waliwasilisha matokeo ya awali ya awamu ya III kwa watendaji wa maendeleo wa aina mbali mbali, ikiwa ni pamoja na wizara za serikali, watafiti, wafadhili, watumishi wa mashirika yasiyo ya serikali (NGOs), na watumishi wa mipango wa Oxfam, wakati wanawake wakulima wadogo wadogo walikuwepo ili kushirikisha uzoefu wa ushiriki wao katika vikundi vya nguvu za pamoja. Timu ya mradi ilikusanya mrejesho kuhusu matokeo, pamoja na maoni na mapendekezo kwa uchambuzi zaidi, na washiriki walijadili jinsi matokeo yanavyopasa kuelekeza mikakati ya watendaji wa maendeleo na sera kusonga mbele. Semina za kikanda pia zilifanyika Tanzania na Ethiopia, ambapo walishirikishana jumbe muhimu za mradi na kukusanya mrejesho kutoka kwa wadau muhimu katika maeneo ambapo utafiti ulifanyika. Zaidi ya washiriki 200 kutoka mashirika kama 90 walishiriki katika semina hizo.

Kwa taarifa zaidi kuhusu semina za kitaifa tembelea:

http://womenscollectiveaction.com/National+Seminars

Semina Kitaifa na Bamako, Mali

Kwa taarifa zaidi kuhusu mradi, tembelea:
www.womenscollectiveaction.com

rasilimali unazoweza kupata ni pamoja na: (Taarifa ya Utafiti ya Shirika la Kimataifa la Oxfam kuhusu matokeo na mapendekezo; visa mafunzo vya nchi husika; mawasilisho kuhusu jumbe muhimu kutoka katika utafiti; rekodi za webinar, mambo mapya kutoka awamu za I na II za mradi.

Wasiliana na: Thalia Kidder, E: tkidder@oxfam.org.uk T: +44 (0) 1865 473 727

OXFAM